# GRADE 4 TOPICAL TRIALS

# KISWAHILI

*This PDF Comprises of Assessment CBC questions arranged topically Covering the whole syllabus for the level.*

HARAMBEE
REPUBLIC OF KENYA
MINISTRY OF EDUCATION

## For Marking Schemes contact Mr Machuki

## 0724333200 / 0768321553 or

## *Order online at:*

## *www.kenyaeducators.co.ke*

## KENYA EDUCATORS CONSULTANCY

# MAZOEZI YA MADA ZOTE GREDI YA NNE.

# KISWAHILI.

## KIFUNGU CHA 1: NYUMBANI

**Zoezi 1**

(a) Andika maneno yenye silabi za sauti

(a) p

(b) b

(a) t

(b) d

(a) k

(b) g

(a) ch

(b) j

**Zoezi 2**

(b) Tunga sentensi mbili zenye sauti k na g

**Zoezi 3**

(b) Tunga sentensi sahihi ukitumia vitanzandimi vilivyo hapo juu

**Zoezi 4**

Jaza pengo kwa kutumia kitanzandimi kifaacho kutoka kwenye mabano sentensi zilete maana

1. Mama ali __ kwa rinda lake. (doa, toa)

2. ___ amekula ___ lililomea shambani. (gugu, kuku)


3.___ alivua ____katika bahari pana. (baba, papa)

4. Mvulana aliye___ anaji___ kidonda. (kuna, guna)

5.___ ni kiungo ___ kwa chakula. (tamu, damu)

**Zoezi 5**

Andika majina ya picha hizi



**Zoezi 6**

*Soma ufahamu kisha ujibu maswali*

Nyumbani ni mahali ambapo watu huishi. Nyumba yetu ni kubwa Wala si ndogo. Inapatikana katika mtaa wa Kariakoo. Nje ya nyumba yetu kuna bustani kubwa la maua. Ndani ya nyumba kuna sebule iliyopambwa kwa makochi na meza. Watoto wa meza huwekwa kando ya makochi kama pambo.

Kwa makochi na meza. Watoto wa meza huwekwa kando ya makocho kama pambo. Sakafu ya sebuleni huwa safi kwani hupigwa deki kila mara. Chumba changu cha kulala ni kidogo. Kinatoshea kitanda pekee yake. Sanduku langu na vitu vyengine huviweka mvunguni mwa kitanda. Nilikasirika nilipogundua tende guu la kitanda changu limeliwa na mchwa. Itanilazimu ninunue kitanda chengine.

MASWALI

1. Tafuta visawe vya maneno haya

(a) Nyumbani

(b) Hamaki

2. Kitambaa kinachotumiwa kupigia deki sakafu huitwa .

3. Tafuta maanaya meneno haya

(a) Tendeguu

(b) Mvunguni

(c) Bustani

4. Ni kifaa kipi hakipatikani sebuleni?

(a) Kinu

(b) Kochi

(c) Meza

(d) Kiti

5. Kulingana na habari matende guu ya kitanda yalikuwa na kasoro gani?

**Zoezi 7**

Jibu maswali yafuatayo

1. Kifaa cha kukalia kilicho na sponji kina chopatikana sebuleni huitwa___.


2. Fanicha iliyotengenezwa kwa mbao, watu huwekelea sahani zenye vyakula huitwa_

3. Chumba cha kupokea wageni nyumbani huitwa

4. Kitendo cha kusafisha sakafu kwa kitambaa na maji huitwa .

5. Jiko linalotumia mawe matatu na kuni huitwa

6. Kifaa A huitwa nini kwenye picha




7. Andika maana ya maneno haya

(a) Kizingiti

(b) Mvungu


(c) Tendeguu

(d) Globu

(e) Fremu

8. Chombo cha chuma kinachotumiwa kufungia mlango huitwa

9. Sehemu iliyoonyeshwa kwa mshale huitwa



10. Milango yote ya nyumba mpya imetiwa ___ ya kudumu.

**Zoezi 8**

Gani ni nomino katika sentensi hizi

1. Twende shambani tukalime

2. Chui ni mnyama hatari


3. Miti hii ina maembe mengi.

4. Tendeguu za kitanda zimevunjika.

5. Funga mlango kwa tumbuu.

**Zoezi 9**

Tunga sentensi ukitumia vitendo vilivyo kwenye picha





**Zoezi 10**

Pigia kistari kitenzi katika sentensi hizi

1. Soma kitabu chako.

2. Saida alipiga deki sakafu yote.

3. Tulienda sokoni na shangazi jana.

4. Kanze aliwasili salama.

5. Kiti hiki kinakalika vizuri.

**Zoezi 11**

Tumia kivumishi kwa usahihi

1. Kuku __anadona nafaka

(-eupe)

2. Msichana yule ni ___ kama mlingoti. (refu)

3. Vyakula ___ huleta maradhi. (baya)

4. Udongo ___ ni bora kwa mimea. (-eusi)

5. Kalamu ___ haiandiki kwa hati nadhifu. (fupi)

**Zoezi 12**

Andika aya fupi ukitumia vivumishi ukielezea kuhusu : Mimi

# KIFUNGU CHA 2: NISHAMU MEZANI

**Zoezi 1**

Andika majibu ya mazoezi yafuatayo

**Maamkuzi** **Jibu**

1. Hujambo?

2. U hali gani?

3. Alamsiki

4. Shikamoo?

5. Hamjambo?

**Zoezi 2**

**Maagano** **Jibu**

1. Lala unono

2. Siku njema

4. Kwaheri

5. Tuonane kesho

6. Buriani

**Zoezi 3**

Ambatanisha maamkuzi na maahano kwa jibu sahihi

| A. | B |
|---|---|
| 1. Waambaje? | Masalkheri |
| 2. Habari za nyumbani? | Sina la kuamba |

| | |
|---|---|
| 3. Masalheri | Buriani dawa |
| 4. Usingizi mnono. | Nzuri |
| 5. Buriani | Nawe pia |

**Zoezi 4**

Tumia kamusi kuandika maana amaneno haya

1. maamkuzi

2. fyonya

3. hamaki

4. sebule

5. mkopo

**Zoezi 5**

Kamilisha jedwali hili

| Nomino | Kiwakilishi | Sentensi zenye kiwakilishi |
|---|---|---|
| 1. Msichana. | a | Anasoma kitabu |
| Wasichana. | wa | Wanasoma vitabu |
| 2. Chura | ---------- | ---------- |
| Vyura | ---------- | ---------- |
| 3. Uzi | ---------- | ---------- |
| nyuzi | ---------- | ---------- |
| 4. Mpira | ---------- | ---------- |
| Mipira | ---------- | ---------- |
| 5. Yai | ---------- | ---------- |
| Mayai | ---------- | ---------- |

**Zoezi 6**

Kiei ni kielezi

1. Kasim aliimba vibaya.
2. Mwalimu wa darasa ameketi darasani.
3. Kobe hutembea polepole.
4. Wanafunzi walicheza vibaya mpira uwanjani.
5. Bustani lililimwa jana.

**Zoezi 7**

Tunga sentensi ukitumia vielezi hivi

1. Vizuri
2. Vibaya
3. Bovu

**Zoezi 8**

Jaza pengo kwa kutumia kielezi kinachofaa

1. Watoto waliimba wimbo ___.

2. Usitembee ___ utachelewa shule.

3. Ukilia ___ utaumwa na kichwa.

4. Nina anatazama zawadi yake kwa ___.

(Furaha, sana, polepole, nzuri)

# KIFUNGU CHA 3: MAVAZI

**Zoezi 1**

Unda maneno kutokana na sauti

1. t
2. d
3. k
4. g
5. ch


**Zoezi 2**

Andika jibu sahihi

1. Pitia huku nami nipitie kule, tupatane pale
2. Ukinitembelea Nyayo zi salama
3. Tik! Tik! kutwa kucha
4. Parr mpaka mekka
5. Fatuma mchafu

**Zoezi 3**

Ambatanisha mavazi haya kwa majina yao


A
B
Tai
Rinda
Suruali
Chupi
Tai

**Zoezi 4**

Andika umuhimu wa mavazi (4)

**Zoezi 5**

Soma ufahamu huu kisha uibu maswali yafuatayo

Siku moja mama aliniambia twende dukani. llikuwa siku ya Jumamosi. Sikuwa nimeenda shuleni. Nilichukua kikapu kikubwa. Tulikuwa tunaenda kununua nguo za sikukuu ya mashujaa. Tulifika dukani, kulikwa na mavazi mengi sana. Wateja walijaa dukani. Wengi wao walinunua soksi na tai. Wengine walikuwa wakiyatazama hayo mavazi bila kuyanunua. Mama alinunua suruli yangu na rinda la dada yangu Alimnunulia baba suti na soksi. Tuliviweka vitu hivyo kwenye kikapu. Mama alimpa pesa muuzaji. Baada ya kupewa baki yetu ya pesa tulirudi nyumbani.

MASWALI

1. Tafuta maana ya maneno haya

(a) Duka

(b) Wateja

(c) Soksi

2. Kulingana na taarifa ni mavazi gani waliona dukani?

3. Ni mavazi gani aliyonunuliwa baba?

4. Mtu anayeuza bidhaa sokoni au dukani huitwa?

5. Kulingana na taarifa ni kweli kusema kuwa mama__

A. Alimnunulia dada chupi

B. Alijinunulia rinda

C. Alienda dukani

D. Alinunua mavazi yote dukani

**Zoezi 6**

Jaza pengo kwa kutumia viunganishi vifaavyo

na, kwa sababu, lakini, pia

1. Juma alikula ___ hakushiba. (kwasababu lakini, pia)

2. Tulipita mtihani ____ tulifanya bidii. (lakini, na, kwa sababu)

3. Halima __ Dan wanaosha vyombo. (na, lakini, kwa sababu)

4. Waliadhibiwa ___ walivunja sheria za shule. (pia, kwa sababu, na)

5. Nilifua nguo ___ hazikungara. (pia, kwa sababu, lakini)

**Zoezi 7**

Tumia kihusishi kifaacho katika sentensi zifuatazo

(karibu na, mbali na, juu ya, chini ya nje ya, ndani ya)

1. Maji yametekwa na kuwekwa mtungi.

2. Usicheze barabara kuu.


3. Weka vitabu vya hadithi ya meza.

4. Mgeni anapiga hodi ya nyumba.

5. Matunda yalichunwa ya mti.

**Zoezi 8**

Tunga sentensi ukitumia picha zifuatazo ukitumia kihusishi kinachofaa




**Compiled and Distributed by Kenya Educators Consultancy, P.O.BOX 15400-00500, Nairobi. Tel 0724333200, Email: kenyaeducators@gmail.com. ORDER MARKING SCHEMES ONLINE AT: www.kenyaeducators.co.ke or Contact Kenya Educators Consultancy officials 0724333200/ 0795491185/ 0768321553**

**Zoezi 9**

Tumia kihisishi mwafaka

1. ___ Njoo unisaidie. (Lo!, Mamaee!)

2. ___ tumeshinda mpira wa Kandanda. (Huraah! lo!)

3. ___ umekuwa mtoto mtundu sana. (Lo!, oyee!)

4. ___ tulishangilia kwa furaha tulipofaulu mtihani. (Salale!, Oyee!)

5. ___ mwalimu wetu alikuja kuchelewa shuleni. (Lo!, Mamaee!)

**Zoezi 10**

Tunga sentensi ukitumia vihisishi vifuatavyo

1. Aka!

2. A fanalek!

3. Salalee!

4. Ala!

4. DIRA

# KIFUNGU CHA 4: DIRA

**Zoezi 1**

Andika majina ya adabu na heshima Kwa maneno yaliyopigiwa mstari

1. Kasisi wetu alikufa jana.
2. Ukinywa maji machafu utaharisha.
3. Chura ameosha chooni.
4. Wanafunzi waliadhibiwa matakoni.
5. Mama mwenye mimba amezaa mtoto.

**Zoezi 2**

Tunga sentensi tano zenye maneno ya adabu uliyopewa

1. Aga dunia_
2. Enda haja ndogo_
3. Kuendesha
4. Mjamzito
5. Mkono wa tanzia

**Zoezi 3**

Soma ufahamu

Hatua za usalama unapotumia mtandao

Ni wazi kama jua kuwa teknolojia nchini imekuwa kwa kiwango kikubwa sana. Aidha, kuna wale wanaotumia teknolijia kutuma ujumbe mfupi. Wengine husoma nakala mbalimbali mitandaoni. Ni jambo la kukata maini kuona baadhi ya Vijana wakitumia teknolojia vibaya. Vijana hupoteza usingizi na kuzembea sababu pj; kusakura matini zisizofaa mitandaoni. Ni jambo la kuhuzunisha unapowaona wengine wakiwasiliana na watu wasio wajua.

Vijana wanatahadharishwa kutowasiliana na watu wasiowajua. Je utafanya nini mtu usiyemjua akikutumia ujumbe mtandaoni? Wazazi wana Jukumu la kuwafunza wana wao jinsi ya kutumia teknolojia vizuri na kwa usalama.

Maswali

1. Ni kweli kusema kuwa teknologia nchini

(a) Imedidimia kimataifa

(b) Imesambaa kwa kiwango kikubwa

(c) Haitumiki tena.

(d) Hutumika kutuma ujumbe mfupi pekee

2. “Ni jambo la kukata maini” ina maana gani?

(a) Kufurahi

(b) Kusherehekea

(c) Kuhuzunisha

(d) Kucheza

3. ‘Wazi kama jua’ ni fani gani ya lugha?

(a) Methali

(b) Tashbihi

(c) Nahau

(d) Vitendawili

4. Taja maana ya maneno haya ukitumia kamusi

(a) Teknolojia

(b) Ujumbe


(c) Mtandao

(d) Kusakura

5. Kwa nini vijana huzembea? __

**Zoezi 4**

Jaze mianya kwenye DIRA




**Zoezi 5**

Jaza nafasi

1. Jua huchomoza upande wa ______ na hatua upande wa ___.

2. Nikiuelekeza uso wangu upande wa mashariki mkono wangu wa kulia utakuwa upande gani?

3. Shule iko upande wa kusini nikiwa nyumbani. Je nyumbani yetu iko upande gani wa dira?

4. Nikisimama kuelekea upande wa magharibi kisogo changu kitakuwa upande gani?

**Zoezi 6**

Andika wingi au umoja

Umoja Wingi

1. Mtoto -------------

2. Mzazi --------------

3. Nahodha -----------

4. ----------- farasi

5. Mbu -----------

**Zoezi 7**

Andika sentensi zifuatazo katika wingi

1. Bata alitaga yai kubwa

2. Rubani anaelekea mashariki

3. Kiroboto aliniganda kwa ngozi

4. Mwalimu amefunza vizuri

5. Mbwa anafukuza paka

**Zoezi 8**

Andika sentensi zifuatazo katika umoja

1. Wapishi walipika vyakula vitamu

2. Wakulima wanalima mashamba makubwa

3. Wafinyanzi wameuza vyungu

4. Wezi wamekamatwa na walinzi

5. Samaki waliopikwa wameliwa

**Zoezi 9**

Andika wingi wa majina haya

**Umoja** **Wingi**

1. Mpera

2. Mlima

3. Mkono

4. Muhula

5. Mwili

**Zoezi 10**

Andika sentensi zifuatazo kwa umoja

1. Miti ya mapera imekatwa
2. Miko imetumika kupikia vyakula
3. Miguu imevishwa viatu vikubwa
4. Mipango hii si mizuri
5. Msiache mianya mikubwa

**Zoezi 11**

Tafuta maneno yenye ngeli ya U-I kwenye mraba

**Zoezi 12**

Andika maneno ya ngeli ya li-ya unayoyajua

Umoja. Wingi

1.

2.

3.

4.

5.

**Zoezi 13**

Andika sentensi zifuatazo kwa wingi

1. Kufuli la shule limenunuliwa

2. Darasa limefungwa na mwalimu

3. Jino la mwisho linaniuma

4.Gari linaenda kwa kasi

5. Takia lina foronya

# KIFUNGU CHA 5: USHAIRI

**USHAURI**

**Zoezi 1**

Toa maana ya methali hizi

1. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo

2. Mtoto wa nyoka ni nyoka

3. Mtoto hutazama kisogo cha nina

4. Adabisha mtoto awapo mdogo

5. Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.

**Zoezi 2**

Kamilisha methali A kwa majibu B

| A. | B |
|---|---|
| 1. Mchelea mwana_ kulia hulia | Kutunza |
| 2. Teke la kuku halimwumizi | Watapotea |
| 3. Mwana huwa. | Mwanawe |
| 4. Mwongoe mtoto katika njia | Yeye |
| 5. Wazee wakinyamaza watoto | Inayofaa |

**Zoezi 3**

Soma shairi kisha ujibu maswali yafuatayo

Wazazi

Wanangu nawasalimia,

Habari za mchana,

Ali, Malina Rehema,

Ya mgambo imelia

Nina mengi ya kuwaambia,

Tawafunza sawa sawa,

Kuwatii baba na mama,

Ya mgambo imelia.

Heshimu baba na mama,

Tapata Baraka kwa maulana,

Na maisha yako kwa jumla,

Ya mgambo imelia.

Kakulea malezi mema,

Walee ukongwe ukiwafika,

Mjiepushe laana,

Ya mgambo imelia.

(Na Basma Chigongo)

Maswali

1. Shairi hili lina beti ngapi?

2. Shairi zima lina mishororo mingapi?

3. Andika kibwagizo cha ubeti wa pili.

4. Malenga wa shairi hili ni nani?

5. Andika mshororo wa tatu kwenye beti ya nne:

# KIFUNGU CHA 6: BENDERA YA KITAIFA

**Zoezi 1**

Soma shairi kisha ujibu maswali

Uhuru ulipopatikana,
Na wazalendo mashujaa,
Bendera ilipandishwa,
Naipenda nchi yangu.

Nchi yangu ni Kenya,
Alama yake ni bendera,
Tuwe tayari kuilinda,
Naipenda nchi yangu.

Rangi nne za bendera,

Nyeusi rangi ya watu,

Nyeupe rangi ya amani,

Naipenda nchi yangu.

Nyekundu rangi ya damu,

lliyomwagika kwa vita,

Kijani rangi ya mazingira,

Naipenda nchi ya Kenya.

Maswali

1. Shairi hili lina beti ngapi?
2. Kila ubeti una mishororg mingapi?
3. Rangi za bendera ni ngapi?
4. Andika mshororo wa pili beti ya nne.
5. Andika maana ya rangi za bendera

**Zoezi 2**

Soma ufahamu kisha ujibu maswali

Taifa la Kenya ni miongoni mwa Nchi chache zilizo na mvuto kwa watalii. Mathalan kuna vivutio vingi vinavyopendeza watalil kama wanyama, mapishi, tamaduni za Kenya, mavazi na hata mazingira.

Mathalan kuna jamii ambazo huvalia nguo za kitamadumt kama wamaasai. Mapishi nayo huthaminiwa kama mboga za kienyeji, wali na vyakula vyenginevyo.

Wanyama ni kivutio kikubwa kwa walalii. Wanyama kama ndovu, chul, simba hufurahisha watalil wanaozuru nchi ya Kenya. Yote haya huipatia nchi fedha za kujenga taifa la Kenya.

Maswali

1. Kulingana na aya ya kwanza

A. Taifa la Kenya lina mvuto kwa watalii

B. Taifa la Kenya halina utamaduni mzuri

C. Taifa la Kenya ni dogo sana

D. Taifa la Kenya halina watalii

2. Jamii gani ambazo bado huvalia nguo ze kitamadunia.

3. Kulingana na taarifa ni kipi kivutio kikubwa zaidi kwa watalii?

4. Taja vivutio vinavyopendeza watalii

5. Ni vipi visawe vya:

(a) Ndovu

(b) Taifa

**Zoezi 3**

Andika umoja wa maneno haya

Umoja wingi

1. vyoo
2. vioo
3. vyombo
4. vyerehani
5. vyuma

**Zoezi 4**

Andika sentensi zifuatazo kwa winei

1. Kiatu kiliraruka ngozi
2. Kikapu kile ni kikubwa
3. Chandarua kizuri kimeanikwa nje
4. Kiota kimejengwa mtini.
5. Kijiti kimenidunga.

**Zoezi 5**

Tunga sentensi tano ukitumia majina ya ngeli ki-vi

**Zoezi 6**

Andika wingi au umoja wa maneno haya

| **Umoja.** | **wingi** |
|---|---|
| 1. Giza | |
| 2. Joto | |
| 3. | Jua |
| 4. Hubo | |
| 5. | Bombo |

**Zoezi 7**

Tunga maneno matano ukitumia ngeli ya li-li katika umoja na wingi

# KIFUNGU CHA 7: MATUNDA NA MIMEA

**Zoezi 1**

Tunga sentensi ukitumia nahau hizi

1. Fanya haki
2. Omba kibali
3. Omba ruhusa
4. Taka idhini
5. Piga hodi

**Zoezi 2**

Ambatanisha Nahau na maana

| Nahau | Maana |
|---|---|
| 1. Tia shime | saidia mtu |
| 2. kujifunga kibwebwe | kufanya bidii |
| 3. Piga jeki. | kuheshimu |
| 4. Omba ruhusa | idhini ya kutaka jambo |
| 5. Fanya haki. | himiza mtu |

**Zoezi 3**

Panga nahau hizi katika kundi la raia au maadili

Piga hodi, kujifunga kibwebwe, omba ruhusa, omba kibali, taka idhini, kata kesi

**Zoezi 4**

Ambatanisha mmea na zao lake

1. Mgomba. Nazi

2. Mharagwe Ndizi

3. Mpunga Mchele

4, Mbuyu Haragwe

5. Mnazi buyu

**Zoezi 5**

Tumia kamusi kufafanua matunda yafuatayo


1. Tende
2. Parachichi
3. Nanasi


4. Nazi

5. Kuyu

**Zoezi 6**

Andika majina ya matunda haya






**Zoezi 7**

Soma ufahamu kisha ujibu maswali

Ulikuwa wakati wa likizo. Mimi na wazazi wangu tulimtembelea nyanya yetu kijijini. Tulipofika tulienda shambani. Shamba la nyanya lilikuwa kubwa sana. Tuliona wafanyikazi wa nyanya wakilima, huku wengine wakipalilia miti ya matunda kama vile miparachichi, michungwa na mitofaha. Pia kuna wale waliotumia mbolea kwa mimea ya migomba ili ndizi ziwe na afya nzuri. Ghafla mvua ilinyesha. Sote tulirudi nyumbani kujikinga mvua.

Maswali

1. Mimea gani ya shambani imetajwa kwenye hadithi?

2. Taja shughuli mbalimbali za shambani ambazo zimetajwa katika hadithi?

**Compiled and Distributed by Kenya Educators Consultancy, P.O.BOX 15400-00500, Nairobi. Tel 0724333200, Email: kenyaeducators@gmail.com. ORDER MARKING SCHEMES ONLINE AT: www.kenyaeducators.co.ke or Contact Kenya Educators Consultancy officials 0724333200/ 0795491185/ 0768321553**

3. Taja mazao yanayotokana na mimea iliyotajwa shambani.

4. Andika maana ya maneno haya:

(a) Shamba

(b) Kijijini

(c) Kupalilia

(d) Tufaha

5. Taja umuhimu wa mvua kwa mimea ya nyanya?

# KIFUNGU CHA 8: WANYAMA PORINI

**Zoezi 1**

Ambatanisha visawe vya maneno haya

Neno. Visawe

1. Ngiri Mbogo

2. Ndovu Abu

3. Nyati. Hasimu

4. Adui Nguruwe

5. Baba. Tembo

**Zoezi 2**

Andika neno jingine lenye maana sawa na lile lililopigiwa mstari

1. Watoto wa jirani ni wazembe sana.

2. Mwalimu aliniongelesha kwa ghadhaby.

3. Ngiri ana mbio kuliko ndovu.

4. Mwizi aliyeiba televisheni amefungwa jela

5. Nipe pesa zangu zote

**Zoezi 3**

Tunga sentensi ukitumia visawe vya maneno haya

1. Nyati

2. Baba

3. Msichana

4. Shida

5. Nyanya

**Zoezi 4**

Mchezo wa kuigiza

Soma mazungumzo haya na mwenzako.

Kengele inalia

Leila: (Akionyesha uso wa furaha) Leo ni siku tuliyokuwa tunaisubiri kwa hamu sana.

David: Kweli kabisa. Ni mbuga gani tunazuru leo?

Leila: Kwaniumeshau? Ni mbuga ya Tsavo.

Rukia: Likizo iliyopita, baba yangu alitupeleka kwenye hiyo mbuga.

David: (Akitega sikio) Uliona nini?

Rukia: Niliona wanyama wengi sana, ambao tumesawoma darasani.

David: Kama ndovu, nyati na mbogo?

Leila: David! Nyati ni kisawe cha mbogo. Maneno hayo yana maana sawa.

Mwalimu: (Ghafla mwalimu anaingia darasani kwa hasira) fanyeni haraka muabiri basi.

Maswali

(a) Taja wahusika kwenye mchezo huu.

(b) Ni nini kisawe cha ndovu?

(c) Taja wanyama watano wa porini unaowajua.

(d) Mwalimu alikuwa anapeleka wanafunzi wapi?

(e) Andika aya moja kuhusu mbuga za wanyama.

(f) Kulingana na mchezo wa kuigiza kutega sikio ina maana ya?

**Zoezi 5**

Kamilisha jedwali hili kwa mnyambuliko ufaao

kutenda kutendea kutendwa

1. Soma
2. Cheza
3. Choma
4. Chora
5. Ruka

**Zoezi 6**

Vitenzi hivi vina mnyambuliko wa kauli gani?

1. Andika - kutenda
2. Pitia
3. Pakwa
4. Ona
5. Endea

**Zoezi 7**

Nyambua vitenzi vifuatazo katika kauli ya kutendea

1. Ziba
2. Andika
3. Anguka
4. Ita
5. Bomoa

# KIFUNGU CHA 9: AFYA BORA

**Zoezi 1**

Soma maigizo haya kisha ujibu maswali

Timo: Hujambo Tina?

Tina : Sijambo Timo

Timo : Ningependa unionyeshe hatua za kucheza mchezo wa kandanda.

Tina: Ahaa! Kwanza mchezo huo lazima huchezwa uwanjani.

Timo : Huchezwa na wachezaji wangapi?

Tina : Katika maandalizi, lazima kuwe na timu mbili. Kila timu ina wachezaji kumi na mmoja.

Timo : Baada ya kuandaa timu ya kucheza ninafaa kufanyaje?

Tina: Kila timu inafaaa kusimama upande wake ikiwa imevalia jezi tofauti.

Timo : Yimo : Kisha.

Tina : Firimbi inapolia, wachezaji hupiga mpira kwa miguu hadi pale mpira utakapoingia kwa goli.

Timo : Asante sana Tina.

Maswali

1. Jina jingine la kandanda ni?__
2. Kufanya mazoezi huboresha afya kwa miili yetu. Taja njia zingine tatu za kuboresha afya.
3. Taja njia za kucheza mchezo wa kandanda.
4. Mahali ambapo michezo hufanyika huitwa .
5. Ni nani alitaka kuonyeshwa hatua za mchezo wa kandanda?

**Zoezi 2**

Soma makala haya kisha ujibu maswali

AFYA NJEMA

Afya bora ndio ufunguo wa maisha bora na marefu. Tunapotunza afya zetu, lunaepuka magonjwa ya kila aina. Miongoni mwa yale mambo anayohitaji binadamu kuwa na afya njema ni lishe bora mazingira safi na miili safi. Tunatunza mazingira na kuyaweka safi kwa kufagia na kupanda miti ili tupate hewa safi. Mili yetu inatakiwa ilishwe kila siku. Nguo zetu ziwe safi kila wakati. Isitoshe tusipovaa nguo safi, chawa watakwama kwenye miili yetu. Tule vyakula vyenye protini, wanga na vitamin. Vyakula hivyo vitajenga miili yetu na kutuepusha kwa magonjwa.

Maswali

1. Kulingana na taarifa, ni nini ufunguo maisha marefu?

2. Kwa nini ni muhimu kutunza afya zetu?

3. Taja mambo matatu yanayohitajika kwa mwanadamu kuwa na afya njema?

4. Tunayatunza vipi mazingira yetu?

5. Taja umuhimu mwengine wa miti wa kuboresha afya zetu?

**Zoezi 3**

Andika kinyume vya Nomino hizi

1. Rafiki

2. Mgeni

3. Furaha

4.Mfalme

5. Mzee

**Zoezi 4**

Toa kinyume cha maneno yaliyopigwa mstari

1. Shangazi hupika chakula kitamu.
2. Walimu wa shule yetu ni watanashati.
3. Waliwatembelea maskini jana.
4. Malezi ya mama ni mazuri.
5. Bwana harusi alipewa zawadi nyingi.

**Zoezi 5**

Tunga sentensi ukitumia vinyume vya Nomino ulivyopewa

1. Mrefu
2. Uhuru
3. Ajuza
4. Mavyaa

# KIFUNGU CHA 10: KUKABILIANA NA UHALIFU

**Zoezi 1**

*Jibu maswali yafuatayo*

1. Mtoto wa Chausiku ni mweusi kama. (makaa, maziwa, sukari)

2. Bwana John ni mwalimu mrefu kama .

(mti, twiga, ndovu)

3. Kasisi wetu ni mfupi kama

(mwamba, nyoka, mlingoti)

4. Usiwe na hasira kama za ___ marafiki.

(ng'ombe, samba, mkizi)

**Zoezi 2**

Kamilisha tashbihi hizi

1. Amekonda kama

2. Nimwembamba kama

3 Sauti nzuri kama

4. Mwaminifu kama

5. Mvi ni nyeupe kama

**Zoezi 3**

Tunga sentensi ukitumia tashbihi hizi

1. Mkati kama simba.

2. Mweusi kama mpingo.

3. Mwembamba kama sindano.

4. Nyeupe kama theluji.

**Tathmini 4**

Soma ufahamu kisha ujibu maswali

Unapotembea mjini, chukua tahadhari kubwa sana. Kuna matapeli wanao wahadaa watu mjini. Aidha matapeli hao hujiweka katika makundi ill kusubiria watembezi wanaoonekana wagenl. Pindi wanapowagundua, wao hunasa pesa, simu na vitu vyengine na kukimbia navyo. Pia kuna wale hutumia maneno matamu. Wao hukuandama na ukifika kichochoroni watakupora na kukimbia. Wengine watakupiga na kukuacha umeumia. Iwapo unataka msaada wowote, basi mtafute bawabu au askari akusaidie, Usijitie kwanye shida tupu bure.

Maswali

1. Kulingana na taarifa ni watu gani wanaoiba pesa

2. Mwandishi anatushauri tufanye nini tunapo tembea mijini?

3. Kamilisha: maneno matamu humtoa___ pangoni.

A. samba B. nyoka C. sungura D. mdudu

4. Ni watu gani tunashauriwa tuwafuate tunapotaka msaada?

5. Andika maana ya neno “matapeli’?

**Zoezi 5**

Tambua nyakati zilizotumika katika sentensi zifuatazo

1. Mama alienda kukata kuni.

2. Mpishi ananunua mboga sokoni.

3. Bimbogo atafunza somo la hesabati.

4. Kiti kitavunjika leo.

5. Paka mlafi anamwaga maziwa.

**Zoezi 6**

Geuza sentensi zifuatazo katika nyakati zilizoonyeshwa mabanoni

1. Mwanafunzi huyu anaitwa kaluma (ujao)

2. Juma atajiunga na chuo kikuu cha Nyen (uliopita)

3. Runinga ilinunuliwa Jana. (uliopo)

4. Mfungwa ataachiliwa aende nyumbani (uliopo)

5. Wazee wanacheza mpira chini ya mti. (ujao)

# KIFUNGU CHA 11: MAPATO

**Zoezi 1**

Jaza pengo kwa kutumia majibu haya

(wateja, bidhaa, rafiki ,muuzaji, kibanda, pesa, masaa)

Tulikutana na 1 yangu juma. Alikuwa ametumwa kwa 2 cha muuza mboga. Nilimpeleka kwa 3 huyo na tukampata na 4 wengi sana. Tulisubiri kwa muda mrefu kabla atuhudumie. Jumaa linunua 5 nyingi. Alimpa muuzaji 6 kisha akarudishiwa baki ya pesa zake. Baada ya 7 mawili tuliachana huku tukiahidiana kuonana juma lijalo.

**Zoezi 2**

KUSOMA

Unapotembeatembea katika maduka yaliyo sokoni, ni kawaida kuwaona wauzaji kwenye vibanda. Wauzaji hao huuza bidhaa tofauti tofauti kama maharagwe, mchele, tomato, matunda na mboga. Utawaona wauzaji wakipiga bei na wate'a wao. Kwani riziki ya wauzaji hutokana na wateja wao, wanaponunua bidhaa kwa pesa. Ukibahatika kuongea na wauzaji hao sokoni, utawapata wamewekeza pesa za kulipa serikali za kaunti ili zilipie leseni ya kuuza sokoni. Wengi wa wanunuzi hao wanapopata mshahara, hukimbilia sokoni huku wamebeba vikapu vikubwavikubwa | kununua bidhaaa.

Maswali

1. Taja baadhi ya vyakula vinavyouzwa sokoni kulingana na ufahamu.

2. Mtu anayenunua bidhaa sokoni huitwaje?

3. Kwa nini wauzaji uwekeza pesa zao?

4. Taja maana ya maneno haya.

(a) Wateja

(b) Bidhaa

(c) Riziki

5. Malipo yanayolipwa mfanyikazi mwisho wa mwezi huitwaje?

(Deni, Ada, Mkopo, Mshahara)

**Zoezi 3**

Tunga sentensi ukitumia maneno haya

(a) Nunua

(b) Mteja

(c) Mshahara

(d) Bidhaa

(e) Riziki

**Zoezi 4**

Kanusha sentensi zifuatazo

1. Mimi nitaimba wimbo wa taifa.

2. Wewe ulicheza shuleni.

3. Yeye alienda sokoni peke yake.

4. Tunasoma vitabu vya hadithi.

5. Mpishi yule alipika chakula kitamu.

**Zoezi 5**

Sentensi hizi ziko katika wakati gani?

1. Baba analimia kwekwe shambani.

2. Juma alienda chuo kikuu.

3. Tutapandisha bendera siku ya ijumaa.

4. Nyinyi mlipata hasara nyingi kwa mkasa huo.

5. Mtoto anakunywa maziwa moto.

**Zoezi 6**

Kanusha sentensi zilizo hapo juu

**Zoezi 7**

Andika katika hali ya ukubwa

Wastani. Ukubwa

1. Mti

2. Mto

3. Mji

4. Mke

5. Mtu

**Zoezi 8**

Andika sentensi zifuatazo katika ukubwa 1. Mfu amezikwa.

2. Mto unafurika.

3. Mtu yeyote asiibe pesa.

4. Mji wake ni wa mbali.

**Zoezi 9**

Andika katika hali ya udogo

Wastani. Udogo

1. Mti

2. Mto

3. Mji

4. Mke

5. Mme

**Zoezi 10**

Andika neno lililopigiwa mstari katika udogo

1. Mto una maji matamu.

2. Mke wake ni mzuri.

3. Ada ya mja hunena.

4. Walienda katika mji wa Mombasa.

# MITIHANI TATHMINI YA KISWAHILI

## TATHMINI YA KWANZA

**Sehemu ya A**

*Soma sentensi hizi kwa sauti*

1. Nilifundishwa jinsi ya kuoka keki.

2. Mama alisonga sima kwa mwiko.

3. Tulifungua shule mwezi wa Septemba.

4. Fenesi ni tunda tamu sana.

5. Feni ya kaka ilivunjika.

2. Andika maneno matano yenye sauti

th na dh

**SEHEMU B**

*Soma hadithi hii kisha ujibu maswali*

Hamadi ni mtoto wa miaka sita Anapenda kucheza na wenzake. Hucheza michezo mbalimbali. Mara nyingi huwinda ndege kwa manati. Hamadi pia hupenda kuchezea vigari. Hutengeneza vigari vya kuchezea. Wakati mwengine hufanya mashindano ya vigari. Mara nyingi Hamadi hushinda siku zote. Siku moja alicheza mchezo wa kuruka kamba. Hamadi alifurahia sana mchezo huo. Hata jua lilipokuchwa, alitamani usiku usiingie. Aliufikiria sana mchezo huo hata alipolala akaanza kuota.

Aliota yuko msituni akiona vitu mbalimbali. Aliona miti mingi msituni. Alifurahia sana mazingira ya msitu. Allona wanyama wengi kama vile twiga, nyani na punda milia. Pia aliona simba, chui, nyati na nyoka. Hamadi aliona ndege tetere, chiriku na tausi. Alimkimbiza tausi ili aende nae nyumbani. Alipomkaribia kumkamata tausi aliruka. Aligutuka ndotoni na akajipata ameanguka sakafuni. Mkononi hakuwa na tausi wala unyoya wake! Alicheka alipoona amekamata shati lake.

Maswali

1. Hamadi ana umri wa miaka mingapi?

2. Taja wanyama wanne Hamadi aliwaona kwenye ndoto

3. Ni michezo ipi Hamadi alipenda kucheza

a)

b)

4. Hamadi hutumia nini kuwinda ndege

5. Kwa nini Hamadi alitamani usiku usiingie

6. Jua huchomoza upande wa

7. Hamadi anapocheza mchezo wa mashindano ya gari hufanya nini?

8. Andika ndege waliotajwa kwenye habari.

9. Je, Hamadi aliota kama yuko wapi?

10. Hamadi aliposhtuka kutoka ndotoni alijipata wapi?

**SEHEMU YA C**

1. Andika vitanzandimi vyenye silabi

P

Ch

D

K

B


J

T

G

2.

Andika majina ya vifaa hivi



3. Maneno yafuatayo ni ya aina gani

Mfano

Soma -_ kitenzi

a) Cheka

b) Sebule

c) Haraka

4. Tegua vitendawili vifuatavyo

a) Nifungue nikufunike

b) Huku ng’o na kule ng’o

c) Tik! Tik! Kutwa kucha

5. Andika kivumishi kwa usahihi

a) Mpishi (-fupi)

b) Viazi (-baya)

c) Ukuta (-refu)

6. Pigia mstari vitenzi katika sentensi hizi

a) Watoto walifagia uwanja wa shule.

b) Kiatu kilichokatika kimetengenezwa.

c) Kiti kipi kimeibiwa.

7. Andika mavazi mawili yanayovaliwa na wanaume

**SEHEMU YA D**

*KUANDIKA INSHA*

Andika insha ya kusisimua kuhusu:

NYUMBA YETU

# TATHMINI YA PILI

**SEHEMU YA A**

*Soma kifungu kifuatacho kwa sauti*

Watoto ni viumbe wa mwenyezi Mungu. Viumbe hawa wana haki zao. Watoto wana mahitaji mengi kama vile malezi mema. Ni kweli kusema “mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.” Watoto wafunzwe tabia njema ili waonyeshe adabu na heshima wanapokua. Watoto pia wapewe lishe bora. Wapelekwe shuleni wapate elimu ili waweze kuwa viongozi wa kesho.

**SEHEMU B**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

Siku ya michezo mwaka uliopita ni siku ambaya Chepkemboi hatawahi kuisahau. Siku hiyo Chepkemboi alikuwa ni mmoja wa wale waliokuwa wakishindania bweni letu la Nyati. Chepkemboi alikuwa ndiye aliyekuwa akiongoza katika mbio za mita mia nne. Lo! Lahaula! Lakwata! Chepkemboi alianguka chini na kuumia vibaya. Damu ilimtiririka kutoka kwenye miguu. Maskauti nasi tulikuwa macho na kukimbia mahali hapo mara moja. Mwalimu mkuu pamoja na walimu waliokuwa karibu walikuja hapo moja kwa moja. Mwalimu mkuu alilpomuona chepchumba alianza kuongea na rununu. Kufumba na kufumbua gari la shule lilifika. Chepchumba aliwekwa ndani ya gari na kupelekwa haraka hospitalini. Mimi pamoja na mwalimu wetu wa kiskauti ndio tulimsindikiza mpaka hospitalini.

Huko hospitalini hatukumbeba tena kwani aliwekwa kwenye machela kusukuma mpaka kwa daktari. Katika chumba cha daktari tulipokelewa na muuguzi ambaye alitusaidia kuiweka machela vizuri kwenye chumba hicho. Daktari alivaa glovu na kumkaribia Chepkemboi ili kumpima. Kushika mguu wake, alitoa ukulele mkubwa ishara ya maumivu aliyokuwa nayo.

Daktari alimdunga sindano ya kumpunguzia maumivu. Baada ya haya, daktari alimtuma kwa idara ya (ekisirel) kupigwa picha. Picha iliporudishwa kwa dakatari ilionekana

kwamba mguu wake ulikuwa umevunjika. Daktari aliamrisha afungwe plasta kisha baadaye tukaruhusiwa kurudi nyumbani naye.

Maswali

1. Ni nani hatawahi kuisahau siku ya

michezo mwaka uliopita?

2. Chepkemboi aliwakilisha bweni gani?

3. Ni jambo gani lililotokea chepkemboi akikimbia

4. Mwalimu mkuu alifanya nini ili gari la shule lije?

5. Hospitalini, Chepkemboi alibebwa kwa

6. Andika manufaa mawili ya rununu

7. Eleza kwa nini Chepkemboi alitoa ukulele daktari alipompima.

8. Daktari alimtuma Chepkemboi kwa idara ya ___ ili apigwe picha.


9. Ni sehemu gani.ya mwili ya Chepkemboi iliyovunjika?

10. Daktari aliamrisha Chepkemboi afungwe nini?


**SEHEMU YA C**


*SARUFI*

1. Taja majina ya vifaa hivi vya nyumbani




2. Tunga sentensi ukitumia picha zifuatazo



3. Andika majina ya mianya iliyoachwa




a.

b.

c.

d.

4. Andika maneno haya kwa njia ya adabu

A. Kufa

B. Anakojoa

C. Kuharisha

5. Andika wingi au umoja wa maneno haya

A. Kasuku

B. Mwavuli

C. Magodoro

D. Vidole

6. Jaza pengo

a) Aya moja katika shairi huitwaje?

b) Mstari mmoja katika shairi huitwaje?

c) Mtu anayetunga shairi huitwaje?

d) Mtu anayeimba shairi anaitwa

7. Andika mifano ya vihisishi

a)

b)

c)

**SEHEMU D:**

*andika insha kuhusu*:

AFYA BORA

# TATHMINI YA TATU

**Sehemu A**

*Kusikiliza na kuzungumza*

Soma maneno haya kwa sauti

a) Adhabu

b) Madaha

c) Mzembe

d) Ugonjwa

e) Uhalifu

f) Nyundo

g) Huwekeza

h) Tovuti

i) Tarakilishi

j) Farida

k) Mauzo

**SEHEMU B**

*Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali*

Hadija si tabia yake kufuatana na watu wenye tabia mbaya. Lakini siku moja alikata kauli kwenda katika sherehe za sikukuu ya Madaraka. Aliandamana na watu vichwa maji. Watu hao walimcheka kila mahali. Wengine walisukumana hata na mama wajawazito. Waliwatisha watoto wadogo na kuwangurumia kama simba. Watoto walilia na kukimbia ovyo. Watu wengine walitoa sigara walizozificha mifukoni wakavuta. Hadija alichukia kile kitendo cha watu hao. Alichukia nywele zao chafu zilizosokotana kama manyoya ya kondoo. Aliyachukia mavazi yao yasiyo na adabu.

Baada ya sherehe wanafunzi hao walirudi shuleni. Hadija alienda moja kwa moja hadi majilisini. Alimweleza mwalimu wa zamu mambo yaliyotokea. Mwalimu alimwelezea

mwalimu mkuu. Uchunguzi ulifanywa na ukweli wote walipatikana, watukutu, wajeuri na vichwa maji waliadhibiwa. Je, wewe ni kama Hadija?

Maswali

1. Andika tabia ya Hadijah

2. Hadija aliandamana na watu wa aina gani?

3. Neno vichwa maji lina maana gani?

4. Chumba cha walimu cha kupumzika huitwa

5. Andika maana ya watukutu.

6. Andika vitendo vitatu Hadija alivyovichukia kulingana na hadithi.

7. Neno sawa na waliandamana ni

(Walifuatana, Walicheza, Walilla, Walislkitika)

8. Hadija alikuwa anaenda sherehe gani?

9. Ni akina nani waloadhibiwa? ___ na ___

10. Kichwa mwafaka cha nakala hii ni

**SEHEMU C**

*SARUFI*

1. Kamilisha methali zifuatazo

a) Mtoto wa nyoka ni ___

b) Mtoto umleavyo ndivyo __

c) Samaki mkunje angali __

2 Chora na upake rangi vifaa vitatu ) vya nyumbani

3. Pigia mstari vitenzi katika sentensi hizi

a) John analima kwekwe.

b) Mwalimu huyu anasahihisha vitabu.

c) Simba mkali amenguruma kwa sauti.

d) Paka wao amekunywa maziwa.

4. Ambatanisha maamkuzi na jibu sahihi

Maamkuzi Jibu

a) Shikamoo Sina la kuamba

b) Sabalkheri Tunayo

c) U hali gani Marahaba

d) Waambaje Njema

e) Makiwa Aheri

5. Unda sentensi upya kwa kutumia viwakilishi

a) Mpishi huyu anapika chakula kitamu.

b) Kiti kile kitauzwa kwa bei ghali.

c) Milango huo umevunjika tumbuu.

d) Nyuzi zile zimekatika

6. Andika visawa vya maneno yafuatayo

A)Televisheni

b) Ndege

c) Barua

d) Nyati

e) Konde

7. Andika vinyume vya maneno yafuatayo

a) Msichana

b) Rafiki

c) Mzee

d) Shangazi

**SEHEMU D:**

*Andika Insha Kuhusu:*

UHALIFU HAUFAI

MTIHANI WA TATHMINI YA NNE

# TATHMINI YA 4

**SEHEMU A**

*Soma sentensi hizi kwa sauti*

A. Raia wataishi kwa upendo

B. Polisi watakamata wahalifu

C. Wadogo waheshimu wakubwa

D. Mwizi alifungwa pingu

**SEHEMU B**

*Soma barua ifuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo*

SHULE YA MSINGI YA MWANGAZA

S.L.P 422,

KOGELO

06-09-2014

Kwa mjomba,

Pokea salamu nyingi kutoka humu nyumbani. Baba na mama hawajambo. Pia kaka na dadangu ni wazima na wanaendelea vizuri na masomo. Je, huko m wazima?

Nina furaha kukujulisha kuwa nimefanya vizuri mitihani ya darasa la nne na mwalimu wetu amesema kuwa nitaenda darasa la tano mwakani.

Kusudi la kukuandikia barua hii ni kukuomba uje huku nyumbani kwetu usherehekee nasi ufanisi huu wangu masomoni. Kama unavyokumbuka hapo awali nilikuwa nashindwa na masomo lakini sasa nashukuru Mungu. Bidii na maombi yetu sote imezaa matunda mema.

Sherehe zenyewe zitafanyika humu nyumbani mwetu mnamo tarehe ishirini mwezi huu wa kumi na moja. Zitaanza saa nane alasiri, karibu.

Mimi wako

Basma Omari

Maswali

1. Shule ya mwandishi yaitwaje?
2. Shule hii iko wapi?
3. Katika barua hii mtajo ni upi?
4. Anayeandika barua hii ni nani?
5. Je, mwandishi anamwandikia nani barua hii?
6. Ni nini maaana ya mwakani?
7. Maana ya neno kusudi ni
8. Je, mwandishi alikuwa na lengo gani la kuandika barua?
9. Kwanini mwandishi ana sherehe kwao?
10. Sherehe anayoizungumzia mwandishi ni ya lini?

*SEHEMU YA C SARUFI*

1. Kamilisha tashbihi kwa usahihi

a) Mrefu kama

b) Mwembamba kama

c) Mfupi kama

2. Andika ngeli za maneno haya

a) Kufuli

b) Kidole

c) Mpishi

d) Pera

e) Mkate

3. Kanusha sentensi zifuatazo

a) Mimi niliosha ngua zangu.

b) Sisi tutaenda sokoni.

c) Yeye anaimba wimbo.

d) Wao walisoma vitabu.

4. Andika ukubwa wa nomino hizi

a) Mbwa


b) Mtu

c) Mto


d) Mji

e) Mke


5. Andika majina ya mavazi haya


(a)
(b)

(c)



6. Tumia picha kutunga sentensi sahihi ukitumia kihisishi kifaacho



7. Andika majina ya heshima kwa maneno yaliyopigiwa mstari

A. Malenga wa mshairi alikufa Jana

B. Tafadhali mwalimu niruhusu niende chooni

C. Mwalimu wetu amezaa

D. Mama yake ana mimba

**SEHEMU YA D**

*Andika Insha ya kusisimua kuhusu*

SHAMBA LETU

# MTIHANI WA TATHMINI YA TANO

**SEHEMU A**

*Soma kifungu kifuatacho kwa sauti*

Nilizaliwa miaka kumi na moja iliyopita. Wakati huo maisha yalikuwa bado mapya na matumaini yangu yalikuwa mengi sana ingawa nilikuwa bado mtoto mchanga. Kwa upande wa afya nilikuwa nimejaa utovu wa uzima na kuwa kama kigongo. Moyoni nilifurahi sana. Uchovu ulikuwa kitu kigeni mwilini kwani nilikuwa katika mwanzo tu wa maisha yangu.

**SEHEMU B**

*Soma habari zifuatazo kisha uibu maswali yafuatayo*

Kilimo ni shughuli za upanzi wa mimea au ufugaji wa wanyama kwa kutaka kuzalisha mazao. Karibu watu wote nchini Kenya wanategemea moja kwa moja shughuli za kilimo. Hivyo basi tutakuwa hatuendi kombo tukisema kilimo ndicho uti wa mgongo wa uchumi wa taifa letu.

Kuna aina mbili za kilimo; yaani upanzi wa mimea na ufugaji. Aina zote mbili zina faida nyingi mno ufugaji wa wanyama kwa mfano; ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku, nguruwe na wengine wengi ni kazi muhimu. Wanyama hawa humpatia mkulima maziwa. Wanyama hawa humpatia ngozi. Mkulima huvitumia vitu hivi moja kwa moja au pengine huviuza.

Wapo wakulima wengine ambao hufuga nyuki au samaki. Nyuki hutoa asali ambayo ni chakula na hata hutumika kutengezea mishumaa. Samaki nao humpatia mtu protini ambayo husaidia kujenga mwili.

Mkulima hupanda mimea ambayo inatumiwa kwa chakula kama vile mahindi ngano,

mawele na aina nyenginezo za nafaka na mboga. Ipo mimea kama vile kahawa, pamba, Pareto na mingine mingi ambayo hukuzwa ya kuuza.

Maswali

1. Kilimo kinahusu nini?

2. Je, watu wa Kenya hutegemea shughull gani?

3. Je mshumaa hutengenezwa na nini?

4. Kati ya chakula kilichotajwa ni kipi ambacho husaidia mili yetu kukua?

5. Nyuki hufugwa sababu gani?

6. Mahindi, ngano, mawele yote ni aina za

7. Ni aina ngapi za kilimo zilizotajwa kwenye habari?

8. Taja mimea ambayo hukuzwa ya kuuza.

9. Kati ya wanyama hawa ni yupi si mfugo?

(Kondoo, Simba, Ngamia, Ng‘ombe)

10. Nakala hii inazungumzia nini?

**SEHEMU YA C**

*SARUFI*

1. Andika jibu la maamkuzi yafuatayo

a) Shikamoo

b) Masalkheri

c) U hali gani

d) Makiwa

2. Andika maneno matano yaliyo katika ngeli ya U -I

3. JAZA PENGO

a) Mahali pa kukaa ukipumzika au kuwapokea wageni panaitwa

b) Mtu anayetunga shairi anaitwaje?

c) Jiko la kuni huitwa

d) Kitambaa ambacho huwekwa kwenye dirisha kupamba nyumba huitwa

e) Mchi hutumika pamoja na

4. Kamilisha methali hizi .

a) Mchelea mwana kulia hulia


b) paka akiondoka ____

c) Mtoto umleavyo ndivyo ee

d) Mwana akibebwa hutazama _

e) Heshima si_

5. Paka rangi na uandike rangi zilizoonyeshwa kwenye bendera ya Kenya




6. Ambatanisha nahau na maana yake

a) Omba ruhusa__Fanya bidii

b) Fanya haki Idhini ya kutaka jambo

c) Jifunge kibwebwe Tendea haki

7. Andika visawe vya maneno haya

a) Ndovu

b) Shamba

c) Kinyonga

d) Kochi

**SEHEMU D:**

*Andika insha ya kusisimua kuhusu :*

MBUGA LA WANYAMA PORINI

# MTIHANI WA TATHMINI YA SITA

**SEHEMU A**

*Kusikiliza na kuzungumza*

Soma maneno haya

A. Lumbwi

B. Mbogo

C. Alhamisi

D. Uyanywe

E. Muuguzi

F. Maktaba

G. Maradhi

H. Mwenyeji

I. Teknolojia

J. Mfalme

**SEHEMU YA B**

*Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo*

Mamaye Jamila alimaliza kupika chamcha . Yaani chakula cha mchana. Alikuwa amewapikia wanawe ugali kwa kuku.Aliwapakulia watoto wake. Kila mmoja akapata kipande kimoja kikubwa cha kuku na ugali wake.

Aliwaita wakae chumbani wale chakula chao. Jamila alipopewa chakula chake alikataa kukaa na wengine na kutoka nje na chakula chake.

Mara alipotoka nje akaja mwewe na kuchukua nyama yake kutoka sahanini. Jamila alisimama kwa mshangao. Mamayo alipogundua kilichofanyika alimuuliza, “Jamila nyama iko wapi?”

Jamila akakosa la kusema. Alilia na kujuta kwa nini hakumtii mamaye kwa kuketi chumbani kula chakula na wengine.

Maswali

1. Ni nani aliyepika chakula ;

2. Nini maana ya chamcha?

3. Chakula kilichopikwa kilikuwa gani?

4. Ni nani aliyeenda kulia chakula nje?

5. Ni kitu gani mwewe alichochukua?

6. Mwewe ni aina ya ,

(ndege, mnyama, samaki)

7. Unafikiria ni kwa nini Jamila alisimama kwa mshangao?

8. Jamila alionyesha majuto kwa nini?

9. Methali gani inaweza kuelezea yaliyotokea.

10. Tunajifunza nini kutokana na kisa hiki?

**SEHEMU C**

*SARUFI*

Andika wingi wa maneno haya

Umoja Wingi

a) Giza

b) Joto

c) Jua

d) Kinu

e) Embe

f) chura

*Andika nyakati za sentensi zifuatazo*

2. Andika nyakati za sentensi zifuatazo

a) Mimi nitasuka nywele za mama.

b) Tulifunga shule siku ya ijumaa.

c) Ninaenda kumsalimu nyanya.

3. Andika umoja wa sentensi hizi

a) Vichwa vyao vimefungwa plasta.

b) Vyuma vile vimejengewa nyumba.

c) Viungo vilivyopikiwa ni vitamu.

4. Jaza pengo kwa jibu sahihi

a) Mstari mmoja katika shairi huitwa.

b) Kazi ya mnunuzi ni kufanyaje

c) Jibu fa buriani ni

d) Lia, osha, futa na andika ni mifano ya

5. Tumia maneno ya heshima badala ya yale yaliyopigiwa mstarsi

a) Aliyekufa alikuwa mwema

b) Mwanafunzi aliruhisiwa kwenda kukojoa.

c) Matiti yake ni makubwa

d) Alidungwa sindano kwenye matako.

6. Kamilisha vitendawili hivi

a) Anatengeneza chakula lakini hali

b) Mama nieleke

c) Niko lakini hunioni

d) Popote niendapo ananifuata

7. Kamilisha tashbihi zifuatazo

a) Maringo kama

b) Ekundu kama

c) Zito kama

d) Mrembo kama

e) Tumbo kubwa kama

**SEHEMU YA D:**

*Andika insha ya kusisimua kuhusu*:

UHALIFU MBAYA

# TATHMINI YA SABA

**SEHEMU A**

1. Soma sentensi hizi kwa sauti

a) Walimu walifunza somo gani?

b) Lo! Kasisi alipeana msaada wa kutosha!

c) Tulimwaga mjomba alipokuwa akienda Ughaibuni masomoni.

d) Toto lile liliokota dodo kubwa.

e) Mama alipata bata mkubwa sokoni.

f) Alichoka kukata kuni kwa shoka lile.

2. Andika vielezl vitano unavyovijua.

**SEHEMU B**

*Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yafuatayo*

Profesa Wangari Maathai alisifika kote ulimwenguni alipojinyakulia tuzo la Amani la Nobeli la mwaka wa 2004. Profesa huyo alikuwa mwanamke wa kwanza barani Afrika kushinda tuzo hilo. Alikuwa pia Mkenya wa kwanza kabisa kupewa tuzo la amani na nobeli.

Profesa Maathai alitunukiwa tuzo hilo kwa kutambua juhudi zake katika kuhifadhi mazingira na kupigania demokrasia.

Wakati wa kutunukiwa tuzo hilo Maathai alikuwa tayari kutambulikana nyumbani kwao na nchini mwako. Hii ni kwa kuwa wenyeji wa eneo la Tetu, huko wilayani Nyeri anakotoka, walikuwa wamemchagua kuwa mbunge wao. Nayo serikali ilikuwa imemteua kuwa naibu wa waziri wa mazingira. Kweli mcheza kwao hutuzwa.

Maswali

1. Profesa Maathai alisifika wapi?

2. Sifa za Maathai zilienea duniani lini?

3. kati ya sentensi hizi gani ni sahihi?

(i) Alikuwa mwanamke wa kwanza barani Afrika kushinda tuzo ilo

(ii) Kulikuwa na watu wengine barani afrika kushinda tuzo hilo

(iii) Hakukuwa na mkenya mwengine aliyewahi kushinda tuzo hilo

(iv) Alipewa tuzo hilo mwaka wa 2004

4. Tuzo alilotunukiwa Maathai linaweza kuelezwa ni la aina gani?

5. Maathai alitunukiwa tuzo hilo kutokana na juhudi zake katika nini?

6. Je serikali ilikuwa imemteua Maathai kuwa .

7. Maathai ni mzaliwa wa kaunti gani?

8. Kenya ni nchi ilhali Afrikani

(Taifa, Tarafa, Bara)

9. Wenyeji ina maana gani?

10.Mcheza kwao hutuzwa ni aina ya

(Msamiati, methali, nahau, vitendawili)

SEHEMU C

1. Chora, andika jina na upake rangi mavazi yanayovaliwa na wanawake

2. Tunga sentensi ukitumia nahau hizi

a) Taka idhini

b) Piga hodi

c) Piga chafya

d) Kata kamba

3. Geuza sentensi zifuatazo katika nyakati zilizoonyeshwa mabanoni

a) Rula ilivunjika (uliopo)

b) Mimi nilikula chakula (ujao)

c) Kiatu kitaoshwa (uliopita)

4. Nyambua vitenzi hivi katika kauli a kutendwa

a) Kimbia

b) Zima

c) Cheza

d) Tembea

e) Fua

5. Andika maana ya methali hizi

a) Mtoto umleavyo Ndivyo akuavyo

b) Adabisha mtoto awapo mdogo

c) Mchelea mwana kulia hulia yeye.

d) Mtoto wa nyoka ni nyoka

6. Andika maneno haya kwa wingi

a) Chandarua

b) Chura

c) Mwezi

d) Embe

7. Andika ngeli ya maneno haya

a) Mkwezi

b) Mwembe

c) Msumeno

d) Mawe

SEHEMU D:

Andika insha ya kusisimua kuhusu: MWALIMU WANGU

# MTIHANI WA TATHMINI YA NANE

**SEHEMU A**

*Soma kifungu hiki*

Kumekuwa na fununu kuwa ulimwengu huu wa sasa hauna maisha. Haya yote yamesababishwa na matukio yasiyo ya kawaida kote ulimwenguni. Tukitaja machache tu ningependa kuangazia hali ya uchumi. Uchumi ambao ulikuwa ukikua kwa viwango vha asilimia themanini, sasa unadorora kila siku. Usalama wa kitaifa hasa Mashariki ya kati unatishia kuzuia vita vya tatu vya dunia.

**SEHEMU B**

*Soma hadithl ifuatayo kisha ujibu maswali*

Kondoo ni mnyama anayefugwa kwa sababu ya faida zake. Kutoka kwake tunapata nyama laini, ngozi na manyoya. Mtu akiwafuga kondoo wengi huweza kupata faida kubwa sana. Tabia za kodoo humfanya aitwe mjinga. Mtu anapotaka kumtusi mwenzake humwambia kuwa yeye ni mjinga kama kondoo. Hawezl kupotea, huuwawa urahisi. Wakati kondoo mwingine anaposhikwa na chui, wale wengine hutimua mbio.

Lakini baada ya muda mfupi wao hurudi mbio sana mithili ya umeme ili kuangalia yaliyompata mwenzao. Naye chui huwa anawasubiri na kumshika kondoo mwingine na kumfanya kitoweo. Mtindo huu wao wa kukumbia kimbia na kurudi huendelea mpaka kondoo wole wanapouawa Isipokuwa mmoja wao naye hukimbia kama aliyerukwa na akili asipochungwa yeye hupotea kabisa.

Maswali

1. Je, kondoo ni mnyama anayeishi wapi?

2. Taja faida za kondoo kulingana na habari.

3. Taja wanyama wengine wanaofugwa nyumbani.

4. Ni tabia gani za kondoo ambazo humfanya aitwe mjinga?

5. Kwa nini kondoo hufugwa nyumbani?

6. Kichwa mwafaka cha hadithi hii ni

7. Kondoo mmoja akishikwa na chui wengine hufanyaje ?

8. Kondoo wote wanapouawa na chui Yule wa mwisho .

9. Kondoo ni mnyama anayefungwa wapi?

10.Kondoo ana miguu mingapi?

**SEHEMU YA C**

*SARUFI*

1. Kanusha sentensi hizi

a) Shangazi anapika wali.

b) Sisi hula matunda kila siku.

c) Wewe utaandika riwaya.

d) Mimi nililia sana.

e) Kipepeo atapeperuka.

2. Tunga sentensi ukitumia maneno haya

a) Kifaru

b) Mapato

c) Nyundo

d) Mteja

3. Kamilisha methali hizi

a)__ mtoto awapo mdogo.

b)Mtoto wa __ ni ___

c) ___ mmoja haulei mwana.

d) ___ mkunje angali mbichi.

4. Ambatanisha maagano na jibu lake

Maagano Jibu

a) Buriani kwa heri ya kuonana

b) Ndoto njema buriani dawa


c) Alamsiki Binuru

d) Kwaheri ya mafanikio

5.


5. Andika majina ya piach hizi

a)




__________

b)




__________

c.



__________

d.



__________

6. Tunga sentensi ukitumia vivumishi vifuatavyo

A. Kizuri

B. Mfupi

C. Mweusi

D. Mrefu

7. Tegua vitendawili vifuatavyo

a) Bak! Bandika! Bak! Bandua

b) Huku ng'o na kule ng'o

c) Dadangu ana jicho moja

d) Nifungue nikufunike

# MTIHANI WA TATHMINI YA TISA

**SEHEMU A**

*Soma sentensi zifuatazo kwa usahihi*

1.Mchelea mwana kulia hulia yeye.

2. Uchafu ni kitu kisichotufurahisha sisi.

3. Wavulana wale wanapendana kama chanda na pete.

4. Kiti chake amekinunua wapi?

5. Mbwa alimkimbiza mwizi kwa hasira.

6. Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.

**SEHEMU B**

*Soma habari hii kisha ujibu maswali*

Hapo kale paliondokea mzee aliyeitwa Hekima. Alibahatika kumwoa mke mrembo Sana aliyeitwa pendo. Walifanikiwa kupata mtoto wa kiume aliyeitwa Sijui. Sijui alikuwa mtoto mzuri naye babayo Hekima akamlea vizuri ingawaje mafunzo yake hayakufanikiwa. Pendo na mwanawe Sijui waliishi katika jamii iliyoshirikiana vyema. Walishirikiana kwa mema na mabaya. Tegemeo madogo madogo kutokana na mafunzo aliyopata, Sijui alianza kuwajibu wazazi wake vibaya.

Wazee wa kijiji waliitwa kuzungumuza naye ili abadilishe tabia yake yote aliambiwa yaliingilia sikio la kulia na kutokea la kushoto. Baada ya kusumbuana sana nao alimua kurudi nyumbani. Aliporudi nyumbani wazazi wake walimsamehe na akagundua kuwa majuto ni mjukuu.

Maswali

1. Hapo kale paliondokea mzee aliyeitwa nani?

2. Je mke wa Hekima alikuwa na umbo ganl?

3. Pendo na Hekima walipata mtoto wa jinsia gani?

4. Mwana wa Pendo na Hekima aliitwa

5. Ni akina nani walioshirikiana kwa mema na mabaya?

6. Je, Sijui alikuwa na tabia gani mwanzo?

7. Maneno yaliingia sikio la kushota ina maana ya __

8. Ni nani walioitwa ili waje wazungumze na Sijui?


9. Majuto ni mjukuu ina maana ya

10. Habari hii inatufunza nini?

**SEHEMU C**

*SARUFI*

Mavazi haya yanaitwaje



(b)



______________

(c)




______________

(d)



______________

2. Tazama picha hii kisha utaje majina ya sehemu ulizoonyeshwa




3. Chagua kiunganishi kujaza pengo

a) Gari lilianguka ___ lilibeba abiria kupita kiasi

(na, kwa sababu)

b) Mahindi yalipikwa __ hayakuiva.

(lakini, kwa sababu)

c) Baba __ mama walienda sokoni.

(lakini, na)

d) Nilikimbia kwenda shuleni ___ nilichelewa

(lakini, pia)

4. Nyambua vitenzi vifuatavyo

Kutenda Kutendea Kutendwa

a) Chapwa

b)Futa

c)osha

5. Geuza sentensi hizi katika wakati uliopo

a) Wao walifagia uwanja wa shule.

b) Kaluma ataandika darasani.


c) Sisi hucheza kila siku,

d) Wewe ulifagia darasa.

6. Taja vitenzi vinavyohusiana na picha hizi



(b)



(c)



7. Tumia neno la upole badala ya lilopigiwa mstari

a) Mzee huyu anahara

b) Mama ana mimba

c) Mwalimu wetu alizaa mtoto wa kiume

d) Tafadhali mwalimu naweza enda chooni.

**SEHEMU YA D**

*Andika insha kuhusu:*

Shule yetu

# MTIHANI WA TATHMINI YA KUMI

SEHEMU A

1. Soma maneno ha a kwa usahihi

a) Tarakilishi

b) Runinga

c) Mbogo

d) Lumbwi

e) Haya

f) Abu

g) Waraka

2. Tambua visawe vya maneno uliyosoma

**SEHEMU B**

Soma habari hii kisha ujibu maswali yafuatayo

Maswali

1. Wakati wa kiangazi ni wakati gani?

2. Kula chumvi nyingi ni kufanyaje?

3. Neno mwamba lina maana sawa na

4. Taja taabu na shinda zinzaopatikana wakati wa kiangazi.

5. Taja kisawe cha matwana.

6. Mzee aliokoa vipi maisha ya watu waliopata ajali?

7. Kwa nini mzee alihisi uchungu rohoni?

8. Mzee Yule alihuzunika sana na kutafuta njia ya kuokoa maisha ya akina nani ?

9. Wakati wa ajali mzee aliwaarifu akina nani?

10.Mzee alimshukuru nani kumweka hapa mpaka siku hiyo?

**SEHEMU C**

1. Kanusha sentensi hizi

a) Mwalimu atafunza.

b) Mahindi yanapaliliwa.

c) Muuzaji aliuza bidhaa nyingi.

d) Wewe ulikula chakula

2. Andika vinyume vya maneno haya

a) Kijana

b) Mgeni

c) Maskini

d) Binti

3. Geuza maneno haya katika hali ya udoqo

a) Mke

b) Mbwa

c) Mti

d) Mto

4. Andika maneno manne yenye ngeli ya Ll-YA

5. Vitenzi hivi vimenyambuliwa kwa kauli gani?

a) Pikia

b) Pangwa

c) Washia

d) Katwa

6. Tumia vivumishi kwa usahihi

a) Kanga (-eusi)

b) Chandarua (refu)

c) Mayai (-baya)

d) Mtoto (-fupi)

7. Andika maneno yenye silabi hizi

a) Ch

b) J

**SEHEMU D: INSHA**

*Andika insha ya kusisimua kuhusu:*

SIKU YA SHEREHE YA KUZALIWA KWANGU